

TANGAZO



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwalishia watu wote wanaotarajia kufanya Mtihani wa **Kidato cha Nne** (CSEE) na **Maarifa** (QT), mwaka **2023** kama Watahiniwa wa Kujitegemea kwamba;

1. Kipindi cha usajili kwa Watahiniwa wa Kujitegemea kimeanza tarehe **01/01/2023** hadi **28/02/2023**. Ada ya usajili ni Shilingi **50,000/=** kwa Mtihani wa **Kidato cha Nne** (CSEE) na Shilingi **30,000/=** kwa Mtihani wa **Maarifa** (QT). Aidha, watakaojisajili kwa **kuchelewa** yaani kuanzia tarehe **01/03/2023** hadi **31/03/2023** watalipa Shilingi **65,000/=** kwa ajili ya Mtihani wa **Kidato cha Nne** (CSEE) na Shilingi **40,000/=** kwa ajili ya Mtihani wa **Maarifa** (QT) ikiwa ni ada ya kawaida pamoja na faini.
2. Kabla ya kujisajili kwenye mtandao, waombaji wanapaswa kwenda kwenye Vituo vya Mitihani kuchukua namba rejea (**reference numbers**) zinazotolewa **bure** na kufanya malipo ya ada kupitia Posta au Benki kwa kutumia '**Control Number**'.
3. Ufafanuzi kuhusu utaratibu wa hatua za kufuata katika kutengeneza '**Control Number**' na kujisajili, umetolewa katika tovuti ya Baraza la Mitihani la Tanzania: www.necta.go.tz. Aidha, kwa watahiniwa ambao hawataweza kutumia mfumo huo wafike ofisi za Posta au wapige simu **0738785945** kwa msaada zaidi.
4. Waombaji wote wasisitizwa kuhakikisha wanajisajili mapema kwani mfumo wa usajili utafungwa mara baada ya kipindi cha usajili kukamilika.

Imetolewa na:

KATIBU MTENDAJI